



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA
UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA WAKALA WA
USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**



Dar es Salaam -13 JULAI, 2022

**KUWAKUMBUSHA WAWAKILISHI WA MAKAMPUNI YALIYOSAJILIWA NJE YA NCHI
KUWASILISHA MIZANIA YA MWAKA**

(Imetolewa chini ya Kifungu cha 441(2) na (3) cha Sheria ya Makampuni, Sura 212)

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unaendelea na mchakato wa kuhuisha taarifa za Makampuni kwa njia ya Mtandao (Online Registration System). Zoezi hili linaenda sambamba na kusudio la Msajili wa Makampuni kuzifuta kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi ambazo hazioneshi kuendelea kufanya biashara kwa kigezo cha kushindwa kuwasilisha Mizania ya mwaka (Financial Statements) kwa mujibu wa kifungu cha 438 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Hivyo basi, Msajili wa Makampuni alitoa Notisi ya siku 90 tangu tarehe 30 Mei, 2022 kwa Wawakilishi wa Makampuni yaliyosajiliwa nje ya nchi kama yalivyo orodheshwa kwenye tovuti ya BRELA kuthibitisha kama bado kampuni hizo zina ofisi za biashara hapa nchini.

Kampuni ambazo hazijatekeleza matakwa ya Taarifa hii, zitaondolewa katika Regista ya Makampuni yaliyosajiliwa hapa nchini kwa mujibu wa kifungu cha 441 (3) cha Sheria ya Makampuni, Sura 212 ifikapo tarehe 30 Agosti, 2022.

Orodha ya Makampuni yaliyosajiliwa nje ya nchi yanayokusudiwa kufutwa inapatikana kupitia www.brela.go.tz.

**IMETOLEWA NA:
KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**